**Manispaa ya Songea ilivyodhamiria kutokomeza malaria**

SIKU ya Malaria duniani huadhimishwa Aprili 25 kila mwaka ambapo kwa mwaka huu,Kitaifa imeadhimishwa Mkoa wa Lindi, kimkoa Wilaya ya Tunduru na katika Manispaa ya Songea imefanyika katika Kata ya Ruvuma.



Kauli mbiu ya mwaka huu ni "*Zero malaria inaanza na mimi*".
Kauli mbiu hii inamaanisha kila mmoja anajukumu la kuhakikisha ugonjwa wa malaria unafikia zero hiyo ina maana hakuna mtu atakaekuwa anaugua ugonjwa wa Malaria endapo kila mmoja wetu atajikinga kikamilifu na kupata matibabu sahihi.

Mganga Mkuu wa Manispaa ya Songea Dkt.Mameritha Basike anasema kuwa Katika Halmashauri ya Manispaa hiyo bado ugonjwa wa Malaria ni tatizo kubwa, kwa kuwa ni kati ya magonjwa 10 yanayoongoza kwa matibabu ya nje na ndani hususani watoto chini ya miaka mitano na akinamama wajawazito.

“Miongoni mwa dalili za ugonjwa huo ni homa, maumivu ya viungo, mwili kulegea, kichwa kuuma, baridi na kutetemeka, kutapika, kuharisha, maumivu ya kifua, kukosa hamu ya chakula, kuvimba wengu, kuvimba bandama, degedege na upungufu mkubwa wa damu”,anasema Dkt.Basike.

Kutokana na takwimu za Idara ya Afya za mwaka 2018 katika Manispaa ya Songea waliougua ugonjwa wa malaria na kupata matibabu ya nje ni 27,202 ambayo ni sawa na asilimia 9.22 ya wagonjwa wote 295,010 waliopata matibabu ya nje.

Kulingana na takwimu hizo,wagonjwa waliougua ugonjwa wa malaria na kulazwa kwa mwaka 2018 ni 3209 sawa na asilimia 11.09 ya wagonjwa wote 28913 waliolazwa.

Dkt,Basike anasema kuwa Watoto chini ya umri wa miaka 5 waliougua ugonjwa wa malaria na kutibiwa kwa matibabu ya nje walikuwa 9561 sawa na asilimia 7.719, ya wagonjwa wote 123,862 chini ya miaka 5 waliopata matibabu ya nje.

Dkt.Basike anawataja Watoto 6313 chini ya umri wa miaka 5 waliopata matibabu ya ndani, kati yao watoto 1255 walitibiwa na kulazwa kwa tatizo la malaria sawa na asilimia 19.88.



Amevitaja vifo vilivyotokea dhidi ya ugonjwa wa malaria kwa mwaka 2018 ni 323 sawa na asilimia 60.83 ya vifo vyote 531 vilivyotokea kutokana na magonjwa mengine na kwamba Watoto chini ya miaka mitano waliokufa kutokana na ugonjwa wa malaria ni 65 sawa na asilimia 16.71 ya vifo vyote vilivyotokea kwa watoto chini ya umri wa miaka 5 ambavyo ni 389.

“Ni dhahiri kuwa Malaria huathiri Zaidi watoto wenye umri chini ya miaka mitano na kina mama wajawazito kwa sababu katika kundi hili kinga za kupambana na malaria ni kidogo”,anasisitiza Dkt Basike.

Hata hivyo takwimu za mwaka 2017 zinaonesha kuwa waliougua ugonjwa wa malaria walikuwa 48146 sawa na asilimia 3.1 ya wagonjwa 156,479 waliopata matibabu ya nje. Waliougua ugonjwa wa malaria na kulazwa walikuwa 3821 sawa na asilimia 0.14 ya wagonjwa wote 28,136 waliolazwa.

Anavitaja vifo vilivotokea kutokana na ugonjwa wa malaria kwa mwaka 2017 vilikuwa 99 sawa na asilimia 29 ya vifo vyote 341 vilivyotokana na magonjwa mengine na kwamba Watoto chini ya miaka mitano waliokufa kutokana na malaria walikuwa 45 sawa na asilimia 18 ya vifo vyote 244 vilivyotokea kwa magonjwa mengine kwa watoto chini ya miaka mitano.

Katika kupambana na Malaria,Dkt.Basike amesema Halmashauri ya Manispaa ya Songea imekuwa ikikabiliana na changamoto mbalimbali zikiwemo,Baadhi ya jamii katika Manispaa ya Songea kutozingatia maelekezo ya matumizi sahihi ya vyandarua na matibabu sahihi,akinamama kutowahi kliniki mara anapojihisi kuwa mjamzito na hivyo kuchelewa kupata Tiba za tahadhari.

Changamoto nyingine amezitaja kuwa ni baadhi ya jamii kutowahi matibabu mara wanapoona dalili za ugonjwa wa malaria kwenye vituo vya kutolea huduma za Afya na baadhi ya wakazi wa Manispaa ya Songea kutofanya usafi wa mazingira kwenye maeneo yao na hivyo kuwa na mazingira rafiki ya mazalio ya mbu.

Hata hivyo amesema Halmashauri ya Manispaa ya Songea ina mpango wa kuuwa viluilui vya mbu kwenye mazalia ambapo Kwa mwaka 2018 Halmashauri ya Manispaa ya Songea imeuwa viluilui vya mbu kwa kupulizia kwenye mazalia ya wazi (madimwi, mabwawa ya samaki,) mita za mraba 32,000 na mazalia yaliyofunikwa (kwenye makalo )mita za ujazo 50,000 na kwamba Mpango huu ni endelevu.



Dkt.Basike amesema Halmashauri ya Manispaa ya Songea imetenga siku moja katika mwezi kwa ajili ya kufanya usafi wa mazingira ambapo wakazi wote wa Kata 21 na mitaa 95 ushiriki zoezi la Usafi na hivyo kuharibu mazalio ya mbu na sehemu za kujificha mbu wapevu.

"Elimu ya Afya hutolewa kwa Jamii na wataalamu wa Afya katika Vituo vya kutolea huduma za Afya kwa kushirikiana na Wahudumu wa Afya ya msingi kutoka shirika la ROA",alisema.

Amesema tiba ya tahadhari kwa akina mama wajawazito kwa kipindi cha 2018 walipata akina mama wajawazito 4929 sawa na asilimia 57 kati ya akina mama wajawazito 8680 waliohudhuria kliniki.

Amesema Usambazaji na ugawaji wa vyandarua vyenye dawa ya muda mrefu kupitia mpango wa vyandarua shuleni unafanyika kila mwaka ambapo mwaka 2017 vyandarua 39,062 viligawiwa kwa watoto wa shule za msingi 81, darasa la 1,2,3,5 na la 7.

“kwa sasa Halmshauri ya Manispaa ya Songea inaendelea kugawa vyandarua kwa walemavu 20 kila kata ambapo kwa leo katika maadhimisho ya siku ya malaria duniani walemavu 20 wa kata ya Ruvuma watapewa vyandarua”,alisisitiza.

Amesema Manispaa ya Songea inathamini mchango wa wadau mbali mbali katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa malaria ambao ni Jonh Hopkin University ambao wanagawa vyandarua shule za Msingi, USAID BORESHA AFYA ambao wanafuatilia ubora wa huduma kwenye vituo vya kutolea huduma za Afya na ROA ambao wanatoa elimu ya udhibiti wa malaria ngazi ya jamii.

Katika kukabiliana na malaria,Dkt.Basike amesema Halmashauri inaendelea kujiwekea **mikakati** endelevu ya kupambana na ugonjwa wa malaria ikiwemo,Kushirikiana na Serikali Kuu kuendesha zoezi la mpango wa ugawaji wa vyandarua shuleni, kwa akina mama wajawazito na watoto wanapopata chanjo ya surua wenye umri wa miezi 9.

Mikakati mingine ni Kuendelea kununua dawa, Vipimo (MRDT) vya kutosha vya kupimia Malaria na kusambaza kwenye vituo vya kutolea huduma za Afya na Utoaji elimu kwa jamii kuhusu matumizi sahihi ya vyandarua, kupima kabla kutibiwa, kuwahi matibabu mara unapoona dalili za malaria, kuwahi kliniki na kuweka mazingira katika hali ya usafi.

Dkt.Basike anaitaja mikakati mingine kuwa ni Kuendelea kushirikisha wadau mbalimbali katika kudhibiti ugonjwa wa malaria,Kuendelea kutoa tiba tahadhari kwa akina mama wajawazito ,Kufanya ufuatiliaji,usimamizi na tathimini ya mwenendo wa ugonjwa wa malaria,Kufanya zoezi la utambuzi wa mazalia ya mbu kwenye kata zote na kupulizia dawa ya kuuwa viluilui vya mbu na Kuendelea kuwachukulia hatua za kisheria kwa wakazi wanaokiuka Taratibu, Kanuni na Sheria za Afya na Usafi wa Mazingira.

**Makala haya yameandaliwa na Albano Midelo**
**Afisa Habari Manispaa ya Songea**
**Simu 0784765917**